# Mgogoro wa Hali ya Hewa ni Mgogoro wa Haki za Mtoto

# Kuanzisha Kielezo cha Hatari ya Hali ya Hewa ya Watoto

Huu utafsiri wa Muhtasari wa Utendaji wa ripoti hii umeundwa kwa kushirikiana na limate Cardinals. Climate Cardinals ni shirika lisilo la faida linaloongozwa na vijana wa kimataifa linalotafsiri utafiti na habari ya mabadiliko ya hali ya hewa katika lugha nyingi ili waweze kufikia vijana na viongozi wengi kadri iwezekanavyo.

Cliamte Cardinals wamekubali kufanya tafsiri ya ripoti hii ya UNICEF kwa lugha ambazo sio lugha rasmi za Umoja wa Mataifa. UNICEF inakaribisha mipango hii lakini kumbuka kuwa tafsiri zimeandaliwa chini ya jukumu la Climate Cardinals. UNICEF haichukui jukumu lolote kwa usahihi wa tafsiri hizi. Katika kufanya kazi ili kufanikisha usambazaji mkubwa zaidi wa ufahamu juu ya UNICEF, UNICEF inafurahi kusaidia Climate Cardinals katika kufanya tafsiri hizi zipatikane.

# Muhtasari wa Utendaji

Mgogoro wa hali ya hewa ni changamoto inayofafanua haki za binadamu na watoto za kizazi hiki, na tayari ina athari kubwa kwa ustawi wa watoto ulimwenguni. Kuelewa ni wapi na jinsi gani watoto wako katika hatari ya kipekee kudhuriwa na mgogoro huu ni muhimu sana kujibu. Kielezo cha Hatari ya Hali ya Hewa ya Watoto kinatoa maoni kamili ya kwanza ya watoto kuwa katika hatari kubwa ya kupata madhara kutoka kwa matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa ili kusaidia kuwapa kipaumbele wale walio katika hatari zaidi na mwishowe kuhakikisha watoto wa leo wanarithi sayari wanamoweza kuishi.

**Tunapingana, na kuvuka, mipaka muhimu sana ya sayari**

Tunavuka mipaka muhimu katika mfumo wa asili wa Dunia, pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, upotezaji wa bioanuwai, na kuongezeka kwa viwango vya uchafuzi wa hewa, udongo, maji na bahari. Hatari za hali ya hewa na mazingira, mishtuko na mafadhaiko tayari zina athari mbaya kwa ustawi wa watoto ulimwenguni. Kadiri mipaka hii inavunjwa, vivyo hivyo usawa wa asili ambao ustaarabu wa binadamu umetegemea kwa kukua na kustawi. Watoto wa ulimwengu hawawezi kutegemea tena masharti haya na lazima wafanye njia katika ulimwengu ambao utakuwa hatari zaidi na usio na uhakika katika miaka ijayo.

**Kutumia data ya hali ya juu ya kijiografia, ripoti hii inatoa ushahidi mpya wa ulimwengu juu ya idadi ya watoto ambao kwa sasa wanakabiliwa na hatari mbalimbali za hali ya hewa na mazingira, mishtuko na mafadhaiko:**

*Matukio ya ghafla na yasiyo ya ghafla:*

- **Watoto milioni 820 (zaidi ya theluthi moja ya watoto ulimwenguni) kwa sasa wako katika hatari kubwa sana ya kuadhiriwa na mawimbi ya joto. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu joto la wastani ulimwenguni linaongezeka, na hali ya hali ya hewa inazidi kuwa mbaya. Mwaka 2020 ulikuwa mwaka wenye joto jingi zaidi kuwahi kurekodiwa.**

- **Watoto milioni 400 (karibu mtoto mmoja kati ya watoto sita ulimwenguni) kwa sasa wako katika hatari kubwa ya kupigwa na vimbunga. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu idadi ya marudio ya vimbunga vyenye viwango vya juu (yaani vya kategoria ya nne na tano) huongezeka, kiwango cha mvua huongezeka, na mifumo ya kimbunga hubadilika.**

- **Watoto milioni 330 (mtoto mmoja kati ya watoto saba ulimwenguni) kwa sasa wako katika hatari kubwa sana ya kuathiriwa na mafuriko ya mito. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu mito ya barafu inayeyuka, na mvua huongezeka kwa sababu ya viwango vya juu vya maji kwenye anga kama matokeo ya joto la wastani kuwa juu.**

- **Watoto milioni 240 (mtoto mmoja kati ya watoto 10 ulimwenguni) kwa sasa wako kwenye hatari kubwa sana ya kuathiriwa na mafuriko ya pwani. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu kiwango cha usawa wa bahari kinaendelea kuongezeka, na zikijumuishwa na kuongezeka kwa dhoruba athari zimeongezeka sana.**

*Mabadiliko ya kuanza polepole:*

- **Watoto milioni 920 (zaidi ya theluthi moja ya watoto ulimwenguni) kwa sasa wanakabiliwa na uhaba wa maji. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu mabadiliko ya hali ya hewa huongeza kasi na ukali wa ukame, upungufu wa maji, ubadilikajibadilikaji wa misimu - na hitaji la maji kuongezeka, inayosababisha kupungua kwa maji ardhini.**

- **Watoto milioni 600 (zaidi ya mtoto mmoja kati ya watoto wanne ulimwenguni) kwa sasa wako katika hatari ya kupata magonjwa yanayosababishwa na wadudu, kama vile malaria na dengue, kati ya mengine. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi kwa sababu uendelevu wa hali ya joto na hali ya hewa kwa mbu na vimelea vinavyosambaza magonjwa haya husambaa.**

*Uharibifu na mikazo ya mazingira:*

- **Watoto bilioni 2 (karibu asilimia 90 ya watoto ulimwenguni) kwa sasa wako katika hatari ya kuathiriwa na uchafuzi wa hewa ambao unazidi 10µg/m$^3$. Hii inaweza kuwa mbaya ikiwa mwako wa mafuta ambao husababisha uchafuzi wa hewa hautapunguzwa.**

- **Watoto milioni 815 (zaidi ya theluthi moja ya watoto ulimwenguni) kwa sasa wako hatarini kwa kusababisha uchafuzi wa mazingira kwa sababu ya athari katika hewa, maji, udongo na chakula. Hii inaweza kuwa mbaya zaidi bila uzalishaji wenye kuwajibika zaidi, matumizi na kuchakata upya bidhaa zinazohusiana na risasi.**

**Ni rahisi zaidi kwa watoto kudhuriwa na mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira kuliko watu wazima kwa sababu kadhaa:**

- Ni wadhaifu zaidi kimwili, na hawawezi kuhimili na kusalimika kutoka majanga kama mafuriko, ukame, hali ngumu ya hewa na mawimbi ya joto.
- Ni wadhaifu zaidi kifiziologia; dutu zenye sumu, kama vile risasi na aina zingine za uchafuzi wa mazingira, huathiri watoto zaidi ya watu wazima, hata kwa viwango vya chini vya kuwa hatarini mwa kudhuriwa.
- Wako katika hatari zaidi ya kifo ikilinganishwa na watu wazima kutokana na magonjwa ambayo yanaweza kuzidishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, kama vile malaria na dengue.
- Wana maisha yao yote mbele yao - wakikosa chochote kama matokeo ya uharibifu wa hali ya hewa na mazingira katika umri mdogo kunaweza kusababisha fursa ya kupoteza maisha.

**Ripoti hii pia inachunguza kwa mara ya kwanza ni watoto wangapi wanaishi katika maeneo ambayo hupata hatari nyingi za hali ya hewa na mazingira zinazoingiliana:**


Jambo linalotatiza hasa ni kwamba hatari hizi zinaingiliana. Hatari hizi za hali ya hewa na majanga, na mabadiliko ya mazingira hayatokei kwa kutengwa. Ukame, mafuriko na hali mbaya ya hewa, pamoja na mabadiliko mengine ya mazingira, hutokea moja baada ya nyingine. Hatari hizi hazichangiani katika kuongezeka tu, lakini pia zinasababisha kutothaminiwa kwa mifuko ya jamii na hivyo kuongeza ubaguzi. Zinaingiliana pia na hatari zingine za kijamii, kisiasa na kiafya, pamoja na COVID-19. Hatari zinazoingiliana mwishowe hufanya sehemu zingine za ulimwengu kuwa hatari zaidi kwa watoto - ikipunguza kwa kiasi kikubwa uwezo wao wa baadaye.

**Pointi muhimu za data kwa hatari zinazoingiliana:**

- **Karibu kila mtoto (>asilimia 99) duniani yuko katika hatari ya kudhuriwa angalau na mojawapo ya hatari hizi za hali ya hewa na mazingira, majanga au mabadiliko ya mazingira**
- **Watoto bilioni 2.2 wanakabiliwa na angalau mbili kati ya hatari hizi kuu za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira**
- **Watoto bilioni 1.7 wanakabiliwa na angalau tatu kati ya hatari hizi kuu za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira zinazoingiliana**
- **Watoto milioni 850 wanakabiliwa na angalau nne kati ya hatari hizi za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira**

- **Watoto milioni 330 wanakabiliwa na angalau tano kati ya hatari hizi kuu za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira zinazoingiliana**
- **Watoto milioni 80 wanakabiliwa na angalau sita kati ya hatari hizi za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira**

**Ramani 1: Hatari za Hali ya Hewa na Mazingira, Majanga na Mabadiliko ya Mazingira Zinazoingiliana**




**Idadi ya Hatari, Majanga au Mabadiliko ya Mazingira:**

Ya Juu Sana (≥5)

Ya juu (4)

Ya Juu-Kiasi (3)

Ya Chini-Kiasi (2)

Ya Chini (1)

Kianzilishi: Ramani hii inachanganya data kutoka: Taasisi ya Rasilimali za Dunia (WRI); Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP); Ripoti ya Tathmini ya Ulimwenguni, UNDRR; Kituo cha Mtandao wa Habari ya Sayansi ya Dunia (CIESIN); Mradi wa Atlasi ya Malaria; Messina et al.; Kraemer et al.; Kitengo cha Utafiti wa Hali ya Hewa, Chuo Kikuu cha Anglia Mashariki; Kikundi cha Uchambuzi wa Muundo wa Anga; na Matarajio ya Idadi ya Watu ya Umoja wa Mataifa (masahihisho ya 2019). Tazama methodolojia kwa maelezo kamili.

**Ukosefu wa watoto kupata huduma muhimu, kama vile afya, lishe, elimu na ulinzi wa jamii, inawafanya wawe rahisi kuambukizwa.**

Sio tu kwamba hatari za hali ya hewa na mazingira zinaathiri vibaya ufikiaji wa watoto kwa huduma muhimu, lakini ukosefu wa watoto kupata huduma muhimu pia hupunguza uthabiti wao na uwezo wao wa kuzoea mazingira, ikiongeza zaidi hatari yao ya kudhuriwa na hatari za hali ya hewa na mazingira. Kwa hivyo, mzunguko mbaya huundwa, unaowasukuma watoto wanaoishi katika mazingira magumu kuingia zaidi katika umaskini wakati huo huo ukiongeza hatari yao ya kupitia hali mbaya zaidi na athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa zinazotishia maisha.

Suluhisho la kipekee la muda mrefu kwa matatizo ya hali ya hewa ni kupunguzwa kwa uzalishaji kwa viwango salama - kufikia sifuri-sifuri ifikapo mwaka 2050 ili tuendelee na mpango wa kutoa joto isiyozidi 1.5°C. Walakini, elimumwendo ya hali ya hewa iko kwa namna ambayo juhudi za

kupunguza itachukua miongo kugeuza athari za mabadiliko ya hali ya hewa, na kwa watoto wa leo, itakuwa imechelewa sana. Isipokuwa tukiwekeza sana katika marekebisho na uimara wa huduma za kijamii kwa watoto bilioni 4.2 wazaliwao zaidi ya miaka 30 ijayo, watakabiliwa na hatari kubwa zinazotishia maisha yao na ustawi wao. Marekebisho yoyote lazima yasimame juu ya tathmini makini ya aina na tabia ya hali ya hewa na hatari ya mazingira, majanga au mabadiliko ya mazingira, vile vile kiwango cha hatari ya kudhuriwa ambamo watoto wanajikuta. Kuelewa udhaifu wa watoto ni muhimu kwa kuelewa kiwango kamili cha hatari za hali ya hewa na mazingira zinazoweza kuathiri ustawi wao, na hata kuishi kwao. Ripoti hii inatoa mfumo wa dhana, zana na tathmini ya awali katika ngazi ya kiulimwengu ya athari ya watoto na uwezo wao wa kudhuriwa kwa urahisi kutokana na hatari za hali ya hewa na mazingira, majanga na mabadiliko ya mazingira - ili kusaidia kutoa kipao mbele kwa wale walio katika hatari zaidi.


**Kuanzisha Kielelezo cha Hatari ya Hali ya Hewa ya Watoto (CCRI: Ripoti hii inachanganya ushahidi huu mpya unaokua na data juu ya uwezo wa watoto kudhuriwa ili kutoa mtazamo wa kwanza wa kuelewesha kikamilifu hatari ya hali ya hewa kwa mtazamo wa mtoto.**

Faharasa ya mchanganyiko ya CCRI ni mfano wa mshtuko mwingi ambao unakusudia kuelezea jinsi watoto wamo hatarini mwa kudhuriwa na baadhi ya majanga na mabadiliko hali ya hewa na mazingira. Ni mfano wa sekta mbalimbali unaotafuta kuwakilisha maoni sawa ya sekta tofauti zinazohusika na ustawi wa watoto, ukizingatia mambo ambayo yanaweza kuchangia, au kuchochea, watoto kukosa mambo kadhaa katika muktadha wa mambo yanayohusiana na hali ya hewa na majanga na mabadiliko ya mazingira.

Mfano huo una muundo wa safu nyingi, ambapo faharisi ya mchanganyiko ya CCRI imejengwa kwa kukusanya seti ya viashiria kwenye nguzo mbili:

- Nguzo 1 inapima kiasi cha kuwemo hatarini mwa kudhuriwa na hali ya hewa na majanga na mabadiliko ya mazingira.
- Nguzo 2 inaelezea uwezekano wa mtoto kudhuriwa.

**Ramani ya 2: Faharasa ya Hatari ya Hali ya Hewa kwa Watoto (CCRI)**




**Faharasa ya Hatari ya Hali ya Hewa na Mazingira kwa Watoto (CCRI):**

Ya Juu Sana
Juu
Ya Juu-Kiasi
Ya Chini-Kiasi
Ya Chini
Hakuna data

Kianzilishi: CCRI imeundwa na viashiria vingi kutoka hatari za Hali ya hewa na mazingira, na majanga na mabadiliko ya mazingira, pamoja na uwezo wa watoto kudhuriwa, angalia ripoti kamili kwa maelezo.

**Ulimwenguni, takriban watoto bilioni 1 (karibu nusu ya watoto ulimwenguni) wanaishi katika nchi zilizo katika hatari kubwa sana, kulingana na CCRI.**

Kwa kuongezea:

- **Sehemu zilizomo hatarini zaidi Duniani zinachangia kidogo kwa mabadiliko ya hali ya hewa - nchi 33 zilizo katika hatari kubwa hutoa chini ya asilimia 10 ya utoaji wa gesi chafu duniani Nchi kumi zenye hatari kubwa zaidi hutoa asilimia 0.5 tu ya utoaji wa gesi chafu duniani.**

- **Nchi karibu zote (29 kati ya 33) kati ya zile zilizo katika-hatari kubwa zaidi huhesabiwa kuwa na hali dhaifu pia**

- **Robo (8 kati ya 33) ya nchi zilizo katika-hatari kubwa zaidi zina viwango vya juu sana ya makazi yao kuhamishwa - na zaidi ya asilimia 5 ya idadi ya watu waliohamishwa**

- **Kati ya nchi zilizo-katika hatari kubwa zaidi hakuna hata moja iliyo na alama ya juu (asilimia >80) ya kupitisha na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya DRR kulingana na Mfumo wa Sendai**

- **Asilimia 40 tu ya nchi zilizo katika hatari kubwa zaidi zimetaja watoto na/au vijana katika Michango yao Iliyoamuliwa Kitaifa (NDCs)**

- **Nchi zilizo hatarini sana zilipokea $ 9 bilioni tu kama mtiririko wa kifedha wa ulimwengu, haswa katika mfumo wa ODA, juu ya utafiti wa nishati safi, maendeleo na uzalishaji.**

- **Zaidi (28 kati ya 33) ya nchi zilizo katika hatari kubwa zaidi zina viwango vya chini sana vya vituo vya ufuatiliaji wa kiwango cha chini cha hewa - chini ya asilimia 10 ya idadi ya watoto wanaishi ndani ya kilomita 50 kutoka kituo cha ufuatiliaji**

**Suluhisho la kipekee la muda mrefu la mabadiliko ya hali ya hewa ni kupunguza uzalishaji wa gesi chafu. Hata hivyo, kuna pia vitendo vingi ambavyo hupunguza kuwepo kwa watoto katika hatari ya kuathiriwa na udhaifu wao wa kuweza kuadhuriwa ambao unaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango chao cha jumla cha kuwa hatarini mwa kudhuriwa na hali ya hewa, kwa mfano:**

**Uwekezaji ambao unaboresha upatikanaji wa huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Usafi (WASH) zinaweza kupunguza kwa kiasi fulani kwa jumla hatari kubwa ya kudhuriwa na hali ya hewa kwa watoto milioni 415.**

Kuboresha ufikiaji wa huduma za WASH kunaweza kujumuisha, kwa mfano, tathmini kamili ya vyanzo vya maji, kuwekeza katika kubadilisha vyanzo vya maji, kutumia nishati mbadala, na kufanya kazi na masoko ya ndani ya nchi na sekta binafsi kuhakikisha kuwa huduma za maji na usafi wa mazingira zimejengwa zikizingatia hatari za hali ya hewa. Inaweza pia kujumuisha kuongeza vifaa vya kuhifadhia maji katika ngazi ya familia, na vile vile miradi mbalimabli ya maji ambayo hutoa maji kwa mahitaji ya nyumbani na maisha. Katika ngazi ya kiwilaya na kitaifa inajumuisha usimamizi, ulinzi na ufuatiliaji kamili wa rasilimali za maji. Uthabiti wa jamii inahusiana sana na uthabiti wa huduma zao za WASH.

**Uwekezaji ambao unaboresha matokeo ya elimu unaweza kupunguza kwa jumla hatari ya hali ya hewa kwa watoto milioni 275.**

Kuwekeza katika elimu endelevu kuna matokeo makubwa sana. Elimu iliyoboreshwa ambayo hujenga maarifa na ustadi itachangia katika kuboresha tabia endelevu na upunguzaji wa uzalishaji hewa chafu kama mtu binafsi, taasisi na jamii. Kuboresha matokeo ya kielimu kunaweza kujumuisha, kwa mfano, kuwekeza katika miundombinu ambayo inaweza kukabiliana na majanga ili kupunguza usumbufu wa muda mrefu kwa utaratibu wa kielimu wa watoto, pia suluhu zinazoongeza ufikiaji kwa urahisi, kama vile kupata elimu kwa njia ya mtandao, na usawa. Usawa katika kufikia mambo ni muhimu kutoka kwa mtazamo wa kijinsia, kutoka kwa mtazamo wa mzunguko wa maisha (kutoka udogoni hadi ujana), na pia kwa watoto wenye ulemavu ambao mara nyingi hutengwa. Kuboresha matokeo ya kielimu pia kunaweza kumaanisha pia kuhakikisha

elimu bora, kama vile kutoa mazingira salama, ya kirafiki, walimu waliohitimu na wenye motisha, na mafunzo katika lugha ambazo wanafunzi wanaweza kuelewa. Hii inamaanisha kuangazia maarifa y hivi karibuni na sayansi juu ya mabadiliko ya hali ya hewa katika mitaala ya kitaifa na pia kuhakikisha kuwa watoto wanapata ujuzi wanaohitaji kufanikiwa maishani. Hizi ni ujuzi zinazofaa kwa siku zijazo za kazi, pamoja na ukuaji wa uchumi wa kijani na maisha ambayo hayawezi kuathiriwa na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira mabaya. Mafunzo yanayotegemea ujuzi pia ni muhimu kwa kuwawezesha watoto, vijana na waalimu kushiriki katika shughuli za kupunguza, kurekebisha hali ya hewa na shughuli za kukabiliana na hali ya hewa shuleni, kuhamasisha watoto kuwa sehemu ya suluhisho la mabadiliko ya hali ya hewa.

**Uwekezaji unaoboresha upatikanaji wa huduma za afya na lishe unaweza kupunguza kwa jumla kiasi fulani ya hatari ya hali ya hewa kwa watoto milioni 460.**

Kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kunaweza kujumuisha, kwa mfano, kuwekeza katika huduma bora za utunzaji kwa mama na watoto wachanga, kudumisha mipango ya chanjo, na kuunga mkono huduma za kinga, ukuzaji na matibabu ya homa ya mapafu, kuendesha, malaria na hali zingine za afya ya mtoto. Inajumuisha pia kutambua vitisho vya afya vinavyobadilika ambavyo watoto wanakabiliwa navyo kama matokeo ya hali ya hewa na mazingira na kuweka kipaumbele kwa jinsi tunavyojibu masuala ya kiafya ipasavyo. Inaweza pia kujumuisha kusaidia afya na ustawi wa vijana na kutoa habari maalumu ya afya kulingana na umri. Zaidi ya hayo, inahitaji kuimarisha mifumo ya afya ili kutoa huduma jumuishi kwa watoto.

**Uwekezaji ambao unaboresha upatikanaji wa usalama wa kijamii na kupunguza kwa kiasi fulani umaskini kunaweza kupunguza kwa jumla hatari kubwa ya hali ya hewa kwa watoto milioni 310.**

Kuboresha ufikiaji wa usalama wa kijamii kunahitaji kufanya kazi kwa kufikia bima ya kiulimwengu ya faida za watoto na familia na pia kuhakikisha kuwa mifumo ya ulinzi wa kijamii inatoa unganisho kwa huduma zingine muhimu katika afya, elimu na lishe na pia nguvukazi ya ustawi wa jamii. Kuboresha mwitikio wa mifumo ya ulinzi wa kijamii ya hali ya hewa ni muhimu kwa hiyo wana nafasi nzuri zaidi ya kuzoea majanga na mabadiliko ya hali ya hewa. Hii inahitaji kuelewa athari zinazoongezeka daima za mabadiliko ya hali ya hewa watoto wanazokabili na walezi wao na kubadili mwitiko wa ulinzi wa kijamii ili kuweza kujibu kwa haraka. Kwa mtazamo wa watoto na familia zao, hii inaweza kusababisha janga la hali ya hewa kuwa usumbufu wa muda mfupi badala ya kusukuma familia katika umaskini wa muda mrefu.

**Matatizo ya hali ya hewa inasababisha matizo ya haki za mtoto.** Inaleta matatizo ya maji ... matatizo ya afya ... matatizo ya elimu ... matatizo ya ulinzi ... na tatizo la kushiriki. Inatishia hasa maisha yenyewe ya watoto. Kwa njia hizi zote, inakiuka haki za watoto - kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto.

Kwa bahati mbaya, huu ni mwanzo tu. Kulingana na IPCC, uzalishaji wa gesi chafu ulimwenguni unahitaji kufikia nusu ifikapo 2030 na kufika sifuri ifikapo 2050 ili kuepuka athari mbaya, lakini nchi nyingi hazifanyi kitu kufikia malengo haya. Kuboresha uthabiti wa huduma ambazo watoto wanahitaji itakuwa kitu cha muhimu bila kujali kesho itatukia nini: hata ikiwa uzalishaji wa gesi chafu ungesimama leo, joto la ulimwengu lingeendelea kuongezeka - likiumiza wale walio hatarini zaidi kwanza. Tunahitaji kuharakisha vitendo vinavyolinda watoto kutokana na athari, na pia kupunguza utoaji gesi chafu - haraka. Kuna suluhisho nyingi zenye ahadi ambazo tungeweza kuchukua - pamoja na suluhisho za asili. Mojawapo ya suluhisho endelevu zaidi ni mpito kuelekea mtindo wa uchumi ambao unatenga ukuaji wa uchumi kutoka kwa matumizi ya mafuta na hivyo kupunguza utoaji wa gesi chafu kwa viwango salama. Lingine ni kushauriana moja kwa moja na watoto wenyewe - watoto na vijana wana maoni muhimu juu ya ulimwengu wanaotaka na wanaohitaji ili kustawi. Ni kwa hatua kama hizi za mabadiliko tu ndio tutaweza kuwaachia watoto sayari wanamoweza kuishi.

*Hati ya Kukataa:*

Huu utafsiri wa Muhtasari wa Utendaji wa ripoti hii umeundwa kwa kushirikiana na Climate CArdinals na Respond Crisis Translation. Climate Cardinals ni shirika lisilo la faida linaloongozwa na vijana wa kimataifa linalotafsiri utafiti na habari ya mabadiliko ya hali ya hewa katika lugha nyingi ili waweze kufikia vijana na viongozi wengi kadri iwezekanavyo.

Cliamte Cardinals wamekubali kufanya tafsiri ya ripoti hii ya UNICEF kwa lugha ambazo sio lugha rasmi za Umoja wa Mataifa. UNICEF inakaribisha mipango hii lakini kumbuka kuwa tafsiri zimeandaliwa chini ya jukumu la Climate Cardinals. UNICEF haichukui jukumu lolote kwa usahihi wa tafsiri hizi. Katika kufanya kazi ili kufanikisha usambazaji mkubwa zaidi wa ufahamu juu ya UNICEF, UNICEF inafurahi kusaidia Climate Cardinals katika kufanya tafsiri hizi zipatikane.